**STATE HOUSE ZANZIBAR**
**OFFICE OF THE PRESS SECRETARY**

**PRESS RELEASE**

**Zanzibar** **04.04.2018**

**RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ametembelea eneo la Mpigaduri linalotarajiwa kujengwa bandari mpya pamoja na eneo la Kinazini linalotarajiwa kujengwa mji wa kisasa ikiwa ni miongoni mwa juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukuza uchumi na kuimarisha maendeleo na ustawi wa jamii.**

Akiwa amefuatana na viongozi mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar Balozi Seif Ali Idd pamoja na Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi, Rais Dk. Shein alifanya ziara hiyo fupi ya kutembelea maeneo hayo ambayo yametengwa maalum kwa miradi hiyo ya ujenzi wa bandari mpya pamoja na mji mpya wa kisasa.

Dk. Shein alitembelea maeneo hayo ambayo yametengwa maalum kwa miradi hiyo ambayo ujenzi wake ni miongoni mwa juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufungua milango zaidi ya kiuchumi sambamba na kuleta maendeleo endelevu kwa Zanzibar na wananchi wake.

Akiwa katika ziara hiyo Dk. Shein aliziagiza mamlaka na taasisi zinazohusika na eneo la pembezoni mwa bahari linaloanzia Bwawani, Mpigaduri hadi Maruhubi kuharakisha matayarisho ya eneo hilo, ili kupisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mizigo utakaofanywa na Kampuni ya Kimataifa ya Uhandisi inayoshughulikia miradi ya Ujenzi wa Bandari na Madaraja Makubwa ya China (CHEC).

Pia, Rais Dk. Shein alitumia fursa hiyo kusisitiza haja kwa Taasisi husika kuwatafutia ufumbuzi wa haraka wananchi wanaofanya shughuli zao katika eneo hilo litakalojengwa bandari mpya kwa kuwapatia eneo maalum lililotengwa huko Kihinani Wilaya ya Magharibi "A" ili kuepuka msongamano wakati wa kuanza kwa mradi huo.

Utekelezaji wa mradi huo wa Bandari mpya ya Mpigaduri unatokana na mazungumzo aliyoyafanya Rais Dk. Shein na Rais Xi Jinping wa China wakati wa ziara yake nchini Tanzania na baadae Dk. Shein alipofanya ziara nchini China ambapo suala hilo lilizungumzwa kwa kirefu na matokeo yake ndio utekelezaji wa mradi huo hivi sasa.

Mapema akitoa maelezo kwa Rais, Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Mustafa Aboud Jumbe alieleza kuwa eneo hilo liko tayari kwa utekelezaji wa mradi huo wa bandari ambapo hatua zote za awali zikiwemo kupimwa kwa eneo hilo zimeshakamilika.

Katibu Mkuu huyo alieleza kuwa eneo hilo linalotarajiwa kujengwa bandari hiyo mpya ya mizigo litakuwa na awamu mbili ambapo awamu ya kwanza litakuwa na ukubwa wa mita 400 na eneo la awamu ya Pili litakuwa na ukubwa wa mita 600.

Aliongeza kuwa changamoto kubwa iliyopo hivi sasa katika Bandari ya Malindi ambayo ina ukumbwa wa eneo lenye mita 240 kuwa dogo, litapatiwa ufumbuzi kwa ujenzi wa bandari hiyo mpya ambapo kukamilika kwake kutapelekea shughuli zote za bandari hiyo ya Malindi kuhamishiwa huko bandari mpya ya Mpigaduri mara itakapokamilika.

Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali, Haji Omar Kheir alimueleza Rais Dk. Shein kuwa tayari eneo maalum limeshatengwa kwa ajili ya wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao hapo Mpigaduri huko Kihinani na wameshakabidhiwa hati kutoka Wizara husika.

Nae Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Ayoub Mohamed Mahmoud amuahidi Rais Dk. Shein kuwa si zaidi ya miezi mitatu wafanyabiashara wa eneo hilo la Mpigaduri watakuwa wameshahama katika eneo hilo na kuhamia katika eneo lililotengwa maalum kwa shughuli hizo huko Kihinani kwa kupisha ujenzi wa mradi huo wa bandari mpya.

Aliongeza kuwa eneo hilo la Kihinani ambalo lina ukubwa wa hekta 1.7 liko tayari na tayari fidia imeshatolewa kwa wananchi wa eneo hilo na kinachoendelea hivi sasa ni kuweka vizuri miundombinu ya barabara, umeme pamoja na kuliweka vizuri eneo litakalowekwa mashine ya kukaushia madagaa kutoka Mradi wa (MIVAP).

Akiwa katika eneo la Kinazini linalotarajiwa kujengwa mji mpya wa kisasa Rais Dk. Shein alipata maelezo kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Mustafa Aboud Jumbe pamoja na Mkurugenzi wa Mazingira Zanzibar, Sheha Mjaja alieleza haja ya kufuatwa kwa taratibu za kimazingira katika eneo hilo ambalo hivi sasa limeota mikoko ambayo hapo siku za nyuma haikuwepo.

Rais Dk. Shein alisema kuwa ujenzi huo unahusisha masuala ya ufukiaji wa bahari, hivyo Mamlaka zinazoshughulikia masuala ya ardhi na mazingira hazinabudi kufanya upembuzi yakinifu mapema, ili kufahamu utaratibu utakaofaa kutumika kuyapeleka maji ambayo baada ya ujenzi huo yatakosa njia zake za asili.

Aidha, aliitaka Wizara ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati kuwafahamisha mapema wananchi wa maeneo ya Kinazini waliovamia na kujenga katika eneo hilo kuwa eneo hilo limetengwa maalum na Serikali kwa ajili ya mradi huo huku akisisitiza haja ya kuanza kupimwa kwa eneo hilo ili kuwekwa tayari kwa mradi huo.

Sambamba na hayo, Rais Dk. Shein aliwapongeza viongozi wote walioshirikiana nae katika ziara hiyo maalum.

**Rajab Mkasaba, Ikulu Zanzibar**

**Postal Address: 2422 Tel.:0777427449. Fax: 024 2231822**
**E-mail: rajabmkasaba@yahoo.co.uk**